# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI

## KIKAO CHA TISA

**10 FEBRUARI, 2023**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI

## KIKAO CHA TISA – TAREHE 10 FEBRUARI, 2023

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma kwa kipindi cha tarehe 01 Julai, 2020 hadi 30 Juni, 2021.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha – Mapitio ya Nusu Mwaka 2022/2023 *[Monetary Policy Statement – Mid – Year Review 2022/2023].*

Taarifa ya Mwaka ya Benki Kuu ya Tanzania kwa Mwaka 2021/2022 *[The Annual Report of Bank of Tanzania for the Year 2021/2022].*

## III. MASWALI:

### OFISI YA WAZIRI MKUU:

**132. MHESHIMIWA DKT. ALICE KARUNGI KAIJAGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali haioni haja ya kutoa elimu kwa Watumishi juu ya ukokotoaji wa mafao.

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**133. MHESHIMIWA ESTHER LUKAGO MIDIMU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Hospitali ya Wilaya itajengwa katika Halmashauri ya Wilaya Meatu kwa kuwa Hospitali iliyopo ina hadhi ya Kituo cha Afya.

**134. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kutenga fedha za kutosha za ujenzi wa barabara za Wilaya ya Same.

**135. MHESHIMIWA FRANCIS ISACK MTINGA (IRAMBA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini mipaka ya Halmashauri ya Mkalama na Iramba itatambuliwa ili kuondoa migogoro Kata za Tumuli, Kinyangiri na Gumanga.

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**136. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni chombo gani kinachodhibiti vyuo binafsi vinavyodahili Walimu nchini.

**137. MHESHIMIWA JEREMIAH MRIMI AMSABI (SERENGETI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha VETA Wilayani Serengeti.

**138. MHESHIMIWA SIMON SONGE LUSENGEKILE (BUSEGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itaanza Ujenzi wa Chuo cha VETA katika Halmashauri ya Wilaya ya Busega.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**139. MHESHIMIWA CONCHESTA LEONCE RWAMLAZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali imechukua hatua gani za kumaliza mgogoro wa muda mrefu kati ya Mbuga ya Rwanyabara na Kijiji cha Bushasha - Bukoba.

**WIZARA YA MADINI:**

**140. MHESHIMIWA MRISHO MASHAKA GAMBO (ARUSHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, nini hatma ya madai ya maslahi ya waliokuwa wafanyakazi wa mgodi wa Tanzanite One.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**141. MHESHIMIWA TAMIMA HAJI ABASS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kutoa elimu kwa jamii dhidi ya udhalilishaji na ukatili wa Watoto.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**142. MHESHIMIWA HAJI MAKAME MLENGE (CHWAKA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inashirikiana vipi na Ofisi ya Makamu wa Rais kuweka mazingira mazuri kandokando ya barabara.

**143. MHESHIMIWA GEORGE RANWELL MWENISONGOLE (MBOZI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini barabara ya Mlowo - Utambalila - Chitete na Utambalila - Kamsamba Km 145 itajengwa kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**144. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kuwapatia Wananchi wa Kyerwa Vitambulisho vya Taifa ili waondokane na adha wanayoipata.

**145. MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO (MOSHI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, nini mpango wa Serikali wa kupambana na majanga ya moto yanayotokea mara kwa mara kwenye masoko nchini.

**146. MHESHIMIWA ABEID RAMADHANI IGHONDO (SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi chenye hadhi ya Wilaya katika Jimbo la Singida Kaskazini.

**WIZARA YA AFYA:**

**147. MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA (SIKONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni kwa nini Serikali isitoe matibabu bure kwa Watoto wenye Ugonjwa wa Selimundu.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**148. MHESHIMIWA TOUFIQ SALIM TURKY (MPENDAE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, kuna mpango gani wa kusaidia Makampuni ya Wazawa yenye mikopo katika Taasisi za Fedha kutokana na athari za UVIKO 19.

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:**

**149. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, ni lini Serikali itaziba nakisi ya uagizaji mafuta ya kula kwa kuruhusu uwekezaji mkubwa katika Bonde la Ziwa Tanganyika.

**WIZARA YA KILIMO:**

**150. MHESHIMIWA ZUENA ATHUMANI BUSHIRI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itajenga Skimu za Umwagiliaji katika Vijiji vya Maore, Mpirani, Kadando na Mheza.

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Kwanza)***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023].*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2023.

## V. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:

## VI. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:

**WAZIRI MKUU:**

## VII. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA AFRIKA MASHARIKI.

**DODOMA**
**10 FEBRUARI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**KATIBU WA BUNGE**